




KICHANGA


HARAKATI ZA NGETI

KIMETENGENEZWA NA
TAI STUDIO

NDANI YA KIJIKIJI CHA UHURU, VITENDO VYA MIMBA ZA UTOTONI, VILISHAMIRI. NGETI ALIYEKUWA ANAFANYA VIZURI DARASANI - ANAPATA UJAUZITO KATIKA UMRI MDOGO NA KUBAKI KUFANYA KAZI ZA NYUMBANI.



BABA NGETI AKAA KIMYA! AKIWA AMEKASIRIKA KWASABABU YA UJAUZITO WA MWANAE.



MARA BAADA YA NGETI KUNLIIA MANENO, RADI KUBWA IKAPIGA.



MARA BAADA YA RADI, NGETI ANAANZA KUSIKIA MAUMIVU TUMBONI.

MAMAAA!
MAMAAA!
BABA!!!. UWI
MAMA YANGU,
TUMBO!

GHAFLA KICHANGA KIKATOKEA.

MIMBA ZA LITOTONI
OYEE!

GHAFLA! NGETI ANA ANGUKA CHINI KAMA MZIGO NA KUZIMIA.

NGETI AKIPIGA KELELE KWA MSHANGAO.

MAMAAAAAAA
AAAAAAA!

PIIIII!

KICHANGA KINAMFUNGUA KOPE ZA
MACHO NA KUMWAMSHA.


TOTOO! AMKA
BACHI TUPIGE
STORI.

NISIKILIZE
WEWE DOGO.


MIMI!

KWANI
NAONGEA
NA
NYANI?

HIVI NAOTA
AU KWELI!
NIMEJIFUNGUA?





UMENUIA MANENO,
NA KUMBUKA HAKUNA
KITU KIKALI KAMA
ULIMI WA BINADAMU.




SI UNATAKA
MIMBA
IPOTEE URUDI
CHULE. UEPUKE
AIBU MTAANI.



NDIO,
SITAKI KUZAA
NIKIWA MTOTO,
NATAKA NISOME,
NIWE...NESI. SITAKI
KUZIHARIBU NDOO
ZANGU.






MARA, NGETI ANASHTUKA, AMEVAA UNIFORM, YUKO KWENYE DUNIA HALISI, KUMBE ALIKUWA NDOTONI.




HII NDOTO MBAYA SANA, NITAJILINDA NISIISHI MAISHA KAMA YALE.



NGETI ALIKUWA NA RAFIKI YAKE WA KIUME FAKI, ALIYEKUWA AKIMSHAWISHI WAFANYE MAPENZI, KWA KUMNUNULIA ZAWADI.


ZAWADI ZAKO HIZI HAPA. TWENDE BASI... LEO UTAFUIDI WEWEE!





USINISHIKE FAKI,
ACHANA NA MIMI.
USINIFUATILIE,
UKIENDELEA MIAKA
THELATHINI
ITAKUHUSU.

**NGETI HAKUWA NA MUDA WA MAJADILIANO, NDOTO ILMIFUNZA
MAKUBWA NA KUMFANYA ASIWAZE MARA MBILI JUU YA MAAMUZI YAKE.**




SINA MUDA WA
KUCHEZEA MAISHA YANGU
NA KUHARIBU NDOTO
YANGU. NI MUDA WA
KUOKOA MABINTI
WENGINE.



ACHANA
NAE USIJE
LIKAWA MAMA
MLEZI MUDA
SI WAKO.
TWENDE
UKANISUKE.

NGETI ALIMFUATA SOFI ALIYEKUWA AKIONGEA NA ZINJA MITHILI YA KUTONGOZANA, KIJANA MTANASHATI ANAYEPENDA KUTOKA NA MABINTI WASHULE. ANAMWOKOA NA KUONDOKA NAE.



NGETI NA SOFI WANAONDOKA WAKIMUACHA ZINJA.


WALIPOFIKA BARABARANI, NGETI NA SOFI WANAKUTANA NA GARI ZURI MITA NNE MBELE YAO.



YAANI!
NIMECHOKA KWELI
LEO.

HUNISHINDI MIMI
SOFI.

GARI LINASIMAMA NA SAUTI YA MWANAUME INAUNGURUMA TOKA NDANI, IKIWAONGELESHA KWA LUGHA YA KILASHAI KWELI.



SOFII, MAMBO MREMBO NA MREMBO MWENZIO. WAREMBO KAMA NYIE KWANINI MNATEMBEA KWA MIGULU NA JUA KALI HILI?

SOFI ALIYEKUWA AMEZOEA KUDANDIA LIFTI ZA ZINJA, ALIKUWA AMEANZA KUCHOKA NA LIVUMILIVU UKAMSHINDA.



NGETI TUPANDE.




TWENDENI NIWAPELEKE MNAPOENDA.

NGETI AKIMVUTA MKONO SOFI WAONDOKE ENEO LILE.



TUMESHAFIKA!
NYUMBANI SIO MBALI




ASANTE!

BILA KUAMINI MACHO YAKE, MWAUNAUME HUYO ALIENDELEA NA SAFARI YAKE HUKU AKILAANI.



WAREMBO
MNAPIGA TEKE
FUKO LA HELA.

SOFI ALIENDELEA KUMHOJI NGETI KWA VITENDO VYAKE VYA KUMZUIA KUONGEA NA KUFURAHIA USICHANA NA WANALUME WANAOMPA MUDA NA MANENO MAZURI.



MIMI NAPENDWA NA WAVULANA NA MABABA, YAANI NI MIMI TU KUCHAGUA LAKINI LEO UMENINYIMA FURSA ZOTE!... KWA NINI?

NIKWAMBIE KITU RAFIKI YANGU, SISI NI MABINTI, NA KATIKA UMRI WETU KUNA WANALUME WASIO NA HAYA, WANATUSAKA KUFANYA MAPENZI NA WANATUMIA KILA NJIA!... LAKINI MATOKEO YAKE NI MIMBA KATIKA UMRI MDOGO. NDOTO ZETU ZITAPOTEA.

NI NYUMA YA NYUMBA YA KINA SOFI.



MARA SIMU INAITA.



SOFI AKIONGEA NA ZINJA KWENYE SIMU.



ZINJA AKIWA ANAONGEA NA SOFI KWENYE SIMU.

ACHA KUMSIKILIZA NGETI WEWE, ANAKUPOTEZA. KAMA HAUTAKI, NIRUDISHIE HIYO SIMU NILIYOKUNUNULIA!... LAKINI UKIJA NITAKUPA HELA.



SOFI AKIMKATIA SIMU ZINJA.

ZINJA, MIMI NI BINTI MDOGO NA NINA NDOTO KUBWA. NITAKURUDISHIA SIMU YAKO!



SOFI AKIANGALIA SIMU YAKE
NA KUSIKITIKA.

SOFI NA NGETI WAKIZUNGUMZA.

RAFIKI YANGU,
ZINJA KIIING'ANG'ANIZI
KAMA CHOTE. ANIACHE
NIENDELEE NA MAMBO
YANGU, KUITWA MAMA
BADO MTOTO SITAKI.

SAFI SANA SOFI,
HUO NDOIO MWENDO NA BADO
WASICHANA WENGINE WASIOJIELEWA,
LAZIMA USHAURI UWAFIKIE.

ZINJA AMEFIKA NA BAJAJI YAKE NA KUANZA KUMSEMESHA SOFI.

NDIYO...
SITAKI TENA
KUJISHUGHULISHA NA
MAMBO HAYO.
NIACHE NISOME.

HEE...
YANI KWELI UMEAMUA
KURUDISHA SIMU. EMBU
ACHA MAMBO YAKO YA
KITOTO.

**UJUMBE WANGU
KWA MABINTI WOTE NI KWAMBA.
ACHA KUJIHUSISHA NA MAPENZI
KATIKA UMRI MDOGO. WEWE ANGALIA
NDOTO ZAKO NA JITAHIDI KUTIMIZA
MALENGO YAKO. VITENDO VYA MAPENZI
HUSABABISHA MIMBA NA MAAMBUKIZI
YA MAGONJWA YA ZINAA. UKIFANYA
MASIHARA NAKUTOKEA!
WASICHANA WASOMI
OYEEE.**



KILE AKIWAZACHO MTU MARA NYINGI HUMTOKEA.
BINTI MDOGO MWENYE UJAUZITO NGETI ANAIOMBA MIZIMU YA WAZEE
IPOTEZE MIMBA YAKE ILI ARUDI SHULE. MIZIMU INASIKILIZA OMBI LAKE NA
TUNALETWA KICHANGA CHAKE, KIKIWA NA UWEZO WA KUONGEA NA
KUHOJI JUU YA MWENENDO WAKE ULIOSABABISHA
KUKATIZA NDOTO ZAKE ZA KIMASOMO.

KITABU HIKI

KIMETENGENEZWA NA **TAI STUDIO** KWA
KUSHIRIKIANA NA SHIRIKA LA **UNFPA** KWA AJILI
YA VIJANA WA RIKA BALEHE KUJIFUNZA NA
KUELEWA KUHUSU ATHARI ZA MIMBA ZA UTOTONI
NA KUJIHUSISHA NA MAPENZI KATIKA UMRI
MDOGO. BAADA YA KUSOMA KITABU HIKI, VIJANA
WA RIKA BALEHE WATAJIFUNZA ATHARI HIZI NA
KUPATA MWAMKO WA KUJILINDA NA KUCHUKUWA
TAHADHARI.

WASHIRIKI

